

Maswali

1. Yesu alisema hadithi juu ya nani?
2. Nini ilifanyika kwa mbegu zilizoanguka kwa njia?
3. Nini ilifanyika kwa mbegu zilizoanguka kwa miamba?
4. Nini ilifanyika kwa mbegu zilizoanguka ndani ya miiba?
5. Nini ilifanyika kwa mbegu zilizoanguka kwa ardhi nzuri?
6. Yesu alisema kwamba hadithi hii ilikuwa na maana gani?
7. Mbegu zilizoanguka kwa njia zilikuwa na maana gani?
8. Mbegu zilizoanguka kwa miamba zilikuwa na maana gani?
9. Mbegu zilizoanguka ndani ya miiba zilikuwa na maana gani?
10. Mbegu zilizozaa mara nyingi kwa ardhi nzuri zina maana gani?

Majibu

1. Mkulima aliyekuwa na mbegu ya kupanda.
2. Ndege zilikula zote.
3. Mizizi hazikuenda chini kwa hivyo juu ilichoma na zikakauka.
4. Miiba ilisonga hizo mimea zikiwa michanga.
5. Hizi mbegu zilizaa mavuno mazuri.
6. Yesu alisema mbegu tofauti ni kama watu wanaomsikia na vile wanaitikia.
7. Watu wenyе hawataki kujifunza neno la Mungu.
8. Watu wenyе wanahaja na Mungu lakini kwa mda mfupi.
9. Watu wenyе wanajifunza kuhusu Mungu lakini wasiwasi ya maisha inawazuia.
10. Watu wenyе wanahaja na kusoma kuhusu Mungu na wanajaribu kutumia waliyoyasoma.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 1 Mwaka wa 2



41 Mfano wa mpanzi

Marejeo

Mathayo 13:1—23


Kiini cha somo

Kuonyesha vile tunatakiwa tuitikie Neno la Mungu.

Maneno maalum

1. Mkulima + shamba + ardhi
2. Mbegu + njia + mimea + miiba
3. Ardhi nzuri + afya + vuna
4. Yesu + masikio + ujumbe wa Mungu
5. Njiani + kutoelewa
6. Mwamba + faida kidogo + hakuna mzizi
7. Miiba + shuguli
8. Ardhi nzuri + vuna
9. Mbegu + Neno la Mungu + sikiliza + elewa + itikia

41.1 Umati wa watu ulikusanyika kando ya bahari tulivu. Yesu aliwambia mfano juu ya mbegu. Kulikuwa na mkulima aliyejkuwa na mbegu nyingi ya kupanda. Mkulima alijaza mbegu mkononi mwake kutoka kwa kikapu halafu alirusha mkono huku na huko akitapakanya mbegu kwenye ardhi mpaka mbali.




41.2 Mbegu zingine zilianguka njiani. Baada ya mkulima kuondoka ndege walikuja na kuzikula. Mbegu zingine zilianguka kwa miamba. Mchanga ulikuwa kidogo. Zikaota kama mimea lakini mizizi haikuenda mbali. Jua lilipochomoza mimea michanga ilikauka. Mbegu zingine zilianguka kwenye miiba. Miiba ilizisonga.

41.3 Mbengu iliyoanguka kwa ardhi iliyotengenezwa vizuri ilioita na kukua. Na vichwa vya hiyo mimea ikawa na afya. Wakati wa kuvuna mbegu hii, moja ilizaa mara mia, ingine mara sitini na ingine mara thelathini.

41.4 Baadaye Yesu aliambia umati, "Mkiwa na masikio ya kusikia, msikie na muelewe." Mkulima na mbegu ni picha ya yaliyoko wakati watu wanasilika ujumbe wa Mungu kwa Biblia.

41.5 Mbegu iliyoanguka njiani ni kutokuwa na tumaini. Njiani ni mahali pa kuganyaga. Aina ya ardhi kama hii inafananishwa na watu wasio na ufahamu au hawana haja na ujumbe wa injili. Wanasiliza neno la Mungu likihubiriwa na wanashahau papo hapo.



41.6 Watu wengine wanasiliza neno kwa makini, waelewe lakini ni kwa mda mfupi tu. Yesu anasema hawa watu ni kama mbegu iliyoanguka kwa miamba. Ni mtu anayesikia neno la Mungu, anakubali kwa furaha, lakini kwa ajili hana mizizi, inachukuwa mda mfupi. Jambo lolote likitokea au shida, anaachana nalo.



41.7 Watu wengine wanasilia neno la Mungu na wanaamua kwamba watafuatilia na kujifunza zaidi. Wanasiliza na kujifunza lakini wana wasiwasi ya malimwengu na vile wanaweza kupata pesa. Hatimaye vile miiba inasonga mimea ndivyo hivyo neno la Mungu linasongwa na wasiwasi ya ulimwengu, inakuwa hana haja tena.



41.8 Lakini kuna watu wenye wanataka kujifunza ukweli wa Mungu na wanataka wautumie kwa maisha yao. Yesu anafurahia mbegu inayozaa mafuno mengi. Mbegu iliyopatwa kwa ardhi iliyotengenezwa vizuri huzalisha sana, kama watu wenye wako tayari na haja ya ujumbe wa Mungu. Wanasilia, wanaelewa na maisha yao inabadilishwa wawe mazuri

41.9 Kwa hivyo tukisikia neno la Mungu, ni kama mbegu imepandwa kwa mioyo yetu. Tutaitikia namna gani kama ujumbe wa Mungu? Tutapuuza kama mbegu iliyoanguka njiani? Tutajifunza lakini tukubali kwa mda mfupi? Tutajifunza na hali tuna wasiwasi ya ulimwengu? Au tuitikie mwito wa Mungu na tujifunze zaidi kuhusu Yeye. Maisha yetu yatabadilika na Yesu atatufurahia.